Moja ya sehemu nyeti ambazo ukiziwezea vizuri utayafanya mahusiano yako yawe na afya, yajae amani, furaha na changamko ni ufundi ama utundu wa kuomba msamaha.

Nimekuwa mwalimu na mshauri wa mahusiano kwa muda sasa, na nimepokea malalamiko ya wanawake na wanaume kuhusu makosa waliyofanya wao na waliofanyiwa na watu wawapendao.

Wanawake wengi wamelalamika sana kwamba wanaume zao hawajui hata kuomba msamaha , sio kwamba wanaume hawasemi samahani hapana! Ila hawajui kuomba msamaha ambao utaridhisha mioyo yao.

Wanawake wengi wameishia kuwaambia wanaume zao kwamba *kwahiyo umerahisiasha tu utadhani hicho ulichokifanya ni chepesi kiasi hicho.*

Wanawake wengi wanahitaji kusikia msamaha ulioshiba haswa, na sio msamaha wa juu juu. Msamaha ambao akiusikia atakuwa hana la ziada zaidi ya kukubali na kusema nimekusamehe.

Ndio maana mwanaume unaweza kusema samahani na bado ukaendelea kununiwa , ni kwamba haitaji samahani yako ila anahitaji namna nyingine ya kuomba radhi ambayo itamkolea na ataifurahia.

Wanawake ni watu wa hisia sana hivyo wakati mwingine mwanaume itamlazimu afanye kitu ili akutane na hisia zake ndipo atambue huyo mwanaume anamaanisha.

Mwanaume hana asili ya kujishusha , hivyo wakati mwingine kutokana na nafasi yake kama kiongozi inaweza kumuwia vigumu kuomba radhi.

Lakini kitu cha muhimu mwanaume unachopaswa kufahamu ni kwamba, moja ya sifa za mwanaume bora na anayejitambua ni kutambua na kuelewa kwa uzuri kabisa namna ya kurekebisha mahali ambapo amekosea au ameteleza, na kufanya marekebisho kwa uzuri.

Mwanaume nikwambie ukweli hapa, kama unataka ufaidi hazina aliyo nayo mwanamke wako basi jifunze ufundi huu wa kuomba msamaha. Kwa sababu wakati mwingine mnaposameehana ndipo unapata hamu ya kuwa na mahaba zaidi na kuyafurahia mahusiano yenu.

Mwanamke hana ujanja ukijua namna ya kumteka kwa maneno yako na vitendo vyako.

Mwanamke anapatikana kwa maneno yako pamoja na vitendo vyako, lakini pia unaweza kumpoteza kwa maneno yako na vitendo vyako pia, yaani njia ile ile uliyo mpata unaweza kumpoteza kwa hiyo pia.

Mwanamke kwa sababu ni mtu wa kujishusha anaweza akawa anakusamehe wakati mwingine hata kwa kumwambia samahani tu, lakini kuna makosa anaweza akaikataa samahani yako na kuhitaji kitu cha thamani zaidi ya neno hilo moja samahani.

Zingatia hiki kitu mwanaume,

Baada ya kuumizwa na watu wanaowapenda wanawake wengi hutumia hali ya kukaa kimya ili kuonyesha maumivu yao. na ukiona ameanza kukupuuza ujue tayari umemuumiza vya kutosha.

Wanawake ni wavumilivu sana , hasa kwa watu wanaowapenda, lakini ukimkuta amebadilika na kuacha kuwa karibu na wewe utambue anamaanisha anahitaji ujiulize kanini sasa ana jitenga nawewe, anahitaji ugundue kosa lako.

Mara nyingi hawezi kusema kwamba umemuumiza na umuombe msamaha ila atatumia lugha ya vitendo na usipomuelewa ataumia zaidi.

Hivyo mwanaume unapaswa uwe makini zaidi juu ya ukimya wa mwanamke wako, maana unaweza kumuuliza kama yuko sawa na akakujibu yuko sawa tu.

Hapana hayuko sawa anahitaji utambue kosa lako na umuombe msamaha.

Huo ni upande wa mwanamke , lakini kwa upande wa mwanaume kesi sio kubwa sana kwa sababu mwanamke amezoea kujishusha na mara nyingi wao ndio hupenda kutumia neno hili samahani.

Lakini kuna wakati unaweza kukwazana na mtu wako na mkatengana au msiwasiliane naye tena, hapa pia sizani mwanaume atakuelewa ukimtumia neno moja tu kwamba nisamehe.

Hapa  pana hitaji nguvu ya ziada ambayo itarejesha hamasa kwa mwanaume ili akupe nafasi tena.

Hivyo ni muhimu ukaujua ufundi huu wa namna ya kuomba msamaha kwa mtu wako na akakuelewa vizuri na akarejesha mahusiano mazuri na wewe tena kwa upya na kwa mahaba zaidi.

Emmanuel minga

0755920171